WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko ya Tabianchi (C-SDTP)

2024 - 2034



"Tija Zaidi, Kipato Zaidi, Ustahimilivu zaidi."

scan hapa kuona booklet

IFAD Investing in rural people

OPEC FUND for International Development

GREEN CLIMATE FUND

AFD

TADB

HEIFER INTERNATIONAL

Kuhusu Mradi

Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko ya Tabianchi (C-SDTP) ni mpango wa kimkakati unaolenga kuleta mageuzi katika mnyororo wa thamani wa maziwa nchini Tanzania kwa kuboresha maisha ya wafugaji wadogo, kuongeza usalama wa chakula na lishe, pamoja na kuimarisha uwezo wa sekta ya maziwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

KIPENGELE	MAELEZO
Muda wa Mradi	Miaka 10 (2024 -2034)
Mtekelezaji Mkuu	Wizara ya Mifugo na Uvuvi
Eneo la Mradi	Tanzania Bara na Zanzibar
Washirika wa Maendeleo	IFAD, GCF, OPEC Fund, AFD na Serikali ya Tanzania
Kaya zinazolengwa	140,000
Wanufaika Watarajiwa	Watu 700,000
Eneo la Msingi	Mageuzi ya tasnia ya maziwa kwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi

Dira

Sekta ya maziwa yenye tija, faida na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, inayoboresha maisha, lishe na ajira.

Lengo Kuu

Kuchangia mabadiliko ya tasnia ya maziwa ili kuboresha maisha ya wafugaji, kuongeza usalama wa chakula, na kupunguza madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi.

Lengo la Maendeleo

Kuboresha kipato, uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na lishe miongoni mwa wazalishaji wadogo wa maziwa na ushiriki wao katika mnyororo shindani na usalama wa tasnia ya maziwa.

Nadharia ya Mabadiliko

HALI YA AWALI	HALI BAADA YA UTEKELEZAJI
Ng'ombe wa maziwa wenye uzalishaji mdogo	Mbari za ng'ombe wa maziwa wenye tija ya juu na wanaostahimili mabadiliko ya tabianchi Kuboresha mbari kupitia teknolojia ya uhamilishaji (Artificial insemination)
Utunzaji hafifu wa Mazingira	Mbari zinazolenga kupunguza hewa ya ukaa na ya methane itokanayo na mifugo Kuboresha usimamizi wa samadi ya mifugo
Uhaba wa malisho	Upatikanaji wa malisho bora kwa mwaka mzima
Uhaba wa maji	Upatikanaji wa maji wa uhakika
Maziwa yenye ubora hafifu	Maziwa salama na yenye ubora wa hali ya juu yapatikanayo kupitia mnyororo wa baridi wa maziwa ulio bora kwenye vituo vya ukusanyaji wa maziwa
Uathirika mkubwa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi	Ufugaji unaostahimili mabadiliko ya tabianchi unaolenga kupunguza hewa chafu ya ukaa na methane
Upatikanaji mdogo wa masoko na utegemezi wa mifumo isiyo rasmi ya uuzaji wa maziwa	Mifumo bora ya ukusanyaji wa maziwa, uongezaji thamani wa mazao ya maziwa na upatikanaji wa masoko ya uhakika
Huduma hafifu za ugani wa sekta ya mifugo	Huduma bora za ugani wa Mifugo kwenye maeneo ya mbari, afya na malisho.
Matumizi hafifu ya teknolojia na ubunifu	Ufugaji unaotumia matumizi sahihi ya teknolojia mbalimbali

Maeneo Makuu ya Mradi

Eneo la 1: Uzalishaji maziwa unaozingatia mabadiliko ya tabianchi na uhimilivu wa mifumo ya wazalishaji wadogo wa maziwa.

Eneo la 2: Minyororo ya thamani shirikishi inayozingatia mabadiliko ya tabianchi, matumizi ya maziwa na sera.

Matokeo Tarajiwa

I. Kuongeza uzalishaji wa maziwa unaozingatia mabadiliko ya tabianchi, tija na uhimilivu wa mifumo ya uzalishaji kwa wafugaji wadogo.
II. Kuboresha upatikanaji wa masoko, uwekezaji wa sekta binafsi na kupunguza athari za uharibifu wa mazingira katika tasnia ya maziwa.

Eneo la Mradi (Mikoa, Wilaya na Kata)



The designations employed and the presentation of the material in this map do not imply the expression of any opinion whatsoever on the part of IFAD concerning the delimitation of the frontiers or boundaries, or the authorities thereof.

Map compiled by IFAD | 29-04-2025

Maeneo ya Utekelezaji Tanzania Bara (Halmashauri 21 na kata 63)


MKOA	WILAYA	MAJINA YA KATA
Arusha	Arusha	Sokoni II, Kiranyi na Ikidinga
	Meru	Kikwe, Maruvango na Uwiro
Iringa	Mufindi	Igowole, Ikongosi na Nyololo
	Iringa	Mgama, Nzihi na Ulanda
	Kilolo	Kata za Image, Mtitu na Ng'uruhe
Mbeya	Mbeya	Ilembo, Tembela na Utengule/ Usongwe
	Rungwe	Kisondela, Lufingo na Ikuti
	Busokelo	Itele, Kambasegela na Mpombo
Njombe	Njombe Mji	Utalingoro, Uwemba na Yakobi
	Njombe(W)	Igongolo, Kichiwa na Mtwango
	Wanging‘ombe	Wanging'ombe, Imalinyi na Mdandu
Tanga	Lushoto	Kwekanga, Kilole na Ngwelo
	Muheza	Amani, Mlingano na Pande Darajani
	Mkinga	Gombero, Mhinduro na Daluni
Morogoro	Kilosa	Madoto, Msowero na Parakuyo
	Morogoro	Bwakira Chini, Ngerengere na Selembata
	Mvomero	Dakawa, Diongoya na Mkindo
Pwani	Mkuranga	Tengelea, Panzuo na Nyamato
	Rufiji	Mkongo, Shela na Ngorongo
Kilimanjaro	Siha	Gararagua, Kashashi na Makiwaru
	Moshi	Mwika Kaskazini,Mbokomu na Marangu Mashariki

Maeneo ya utekelezaji Zanzibar (Mikoa 5, Shehia 75)

MKOA	MAJINA YA SHEHIA
Mjini Magharibi	Bumbwisudi, Dimani, Fuoni, Kama, Kianga, Kibondeni, Kiembesamaki, Kizimbani,Kombeni, Maungani, Mbuzini, Mfenesini, Mwanyanya, Mwera na Shakani
Kaskazini Unguja	Bumbwini, Chaani, D/Mbiji, D/Mtambile, Fujoni, Gamba, Kidoti, Kinyasini, Kitope, Kivunge, Mahonda, Mkokotoni, Mkwajuni, Nungwi na Upenja
Kusini Unguja	Bungi,Charawe, Ghana,Jendele, Machui, Mchangani, Mgenihaji, Mpapa, Mtende, Muyuni, Ndijani; Tunguu,Ubago,Unguja Ukuu na Uzi
Kaskazini Pemba	Chimba, Finya, Juguni, Kifundi, Kiungoni, Kiuyu Minungwini, Makangale, Mchanga mdogo, Mihogoni, Msuka, Mtambwe, Mtemani, Wete, Pandani, Piki, na Sizini
Kusini Pemba	Changaaweni, Chonga, Kendwa, Kengeja, Matale, Mgagadu, Mgogoni, Michenzani, Mkungu, Mtambil, Ole, Shungi, Vitongoji, Wawi na Ziwani

Wanufaika wa Mradi

Jumla ya Kata 140,000 zitanufaika moja kwa moja na mradi huu, sawa na takriban ya watu 700,000 katika eneo la mradi.



Watekelezaji wa Mradi

Sekta / Kundi	Jina la Taasisi
Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	Wizara ya Mifugo na Uvuvi Ofisi ya Waziri Mkuu- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)
Utafiti	Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar (ZALIRI) Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA)
Watoa Huduma	Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) Kituo cha Taifa cha uhamilishaji wa Mifugo (NAIC) Wakala wa Taifa wa Maabara za Mifugo (TVLA)
Miundombinu	Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Wakala wa Barabara Zanzibar (ZANROADS) Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Kituo cha Teknolojia za Kilimo na Uhandisi Vijijini (CAMARTEC)
Fedha na Mikopo	Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB)
Lishe na uhamasishaji wa unywaji wa maziwa	Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB)
Maendeleo ya Ushirika	Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) Heifer Internationa

Mafanikio ya Mradi (Hadi kufikia Juni 30 2026)

- Tumewafikia wafugaji wa ng'ombe wa maziwa **9,019** kupitia vikundi/ vyama vya ushirika **162** katika Halmashauri **26** za mradi.
- Tumezitambua kaya **400** kwa ajili ya mpango wa ugawaji wa ng'ombe kupitia utaratibu wa 'Pokea Zawadi Toa Zawadi'.
- Tumetoa mafunzo ya upandaji na uzalishaji wa malisho kwa wafugaji kutoka kaya **469**.
- Tumesambaza kilo **1,000** za mbegu za malisho kupitia vikundi **19** vya mashamba darasa ya mifugo.
- Tumeanzisha ekar**i 28** za mashamba darasa ya malisho katika maeneo ya mradi.
- Tumetoa mafunzo kwa wakaguzi wa maziwa **28** na kuwapatia vifaa vya kupima ubora wa maziwa.
- Tumeendesha mikutano ya wadau wa sekta ya maziwa katika halmashauri **26** za mradi kujadili changamoto na suluhisho.
- Tumetoa mafunzo ya uhimilishaji kwa wataalamu **35** na kuwapatia vifaa vya kufanyia kazi.

Baadhi ya Mipango ya Kimkakati ya Mradi kwa Mwaka wa Fedha 2026/27

- Ujenzi wa vituo vya karantini vya Kwala na Kisakasaka.
- Ununuzi wa mitambo **3** ya kuzalisha gesi ya Nitrojeni Kimiminika (Liquid Nitrogen).
- Ununuzi wa madume **10** ya kuzalisha mbegu za uhimilishaji kwa ajili ya kuwezesha huduma za uhimilishaji bandia.
- Ukarabati wa vituo **10** vya ukusanyaji wa maziwa.
- Ununuzi wa magari **6** ya maabara zinazotembea (Mobile Laboratory Vehicles).
- Ujenzi wa matenki **4** ya kuhifadhi maji na vituo **8** vya kuchotea maji, pamoja na usambazaji wa maji kwa umbali wa kilomita **57** katika Halmashauri za Siha na Moshi, na uchimbaji wa visima **11** katika Halmashauri za Meru na Arusha.
- Ujenzi na ukarabati wa kilomita **25** za barabara zenye hali duni.

Ungana nasi katika Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa nchini Tanzania

Tovuti

https://www.mifugouvuvi.go.tz

https://www.ifad.org/en/w/projects/2000003937

Mitandao ya kijamii

C-SDTP_Maziwa Tanzania

C-SDTP_Maziwa Tanzania

C-SDTP_Maziwa Tanzania

Mawasiliano

OFISI YA MRADI
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
SLP 2870, Dodoma, Tanzania

Kikuyu Avenue, Jengo la Kambarage Tower, Ghorofa ya 11

Barua Pepe:
csdtp@mlf.go.tz